

HALMASHAURI YA MJI HANDENI

TAARIFA FUPI YA UJENZI WA OFISI YA JENGO LA HALMASHAURI

Ujenzi wa Jengo la Ofisi ulianza tarehe 11 Octoba, 2017 baada ya Halmashauri ya Mji kukabidhiana eneo la ujenzi na Mkandarasi. Jengo linajengwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) chini ya kikosi Maalumu kiitwacho TBA Brigade na Mkandarasi Mshauri ambaye ni TBA Consultant.

Gharama za ujenzi wa Jengo mpaka utakapokamilika utagharimu takribani Tsh **3,619,007,387.00** na mpaka sasa Halmashauri imeshapokea kiasi cha **Tsh 1,550,000,000.00** na imeshalipa kiasi cha **Tsh 500,000,000.00** kwa ajili ya Malipo ya Awali (Advance Payment). Aidha kufikia Machi, 2017 kiasi cha **Tsh 456,796,650.53** kimeombwa na Mkandarasi kwa Hati ya Malipo Namba 02 kwa kazi ambayo imefanyika. Utaratibu wa kulipa fedha hizo unaendelea na hivyo itafanya jumla ya fedha zilizotumika kuwa ni **Tsh 956,796,650.00**

Kazi iliyokamilika mpaka sasa ni *Mobilization* yaani kazi za awali na kazi ya ujenzi wa msingi inaelekea kukamilika. Ujenzi wa mradi unategemea kukamilika baada ya miezi 18 yaani Mwezi Machi, 2019. Aidha ili mradi ukamiliki tunahitaji kiasi cha jumla ya Tsh **4,069,007,388.00** na hivyo kufanya jumla mradi mzima ni Tsh **5,619,007,388.00**. Gharama hizi zimeongezeka kutokana na :-

- (i) Uvunaji wa Maji ya Mvua **Tsh 1,000,000,000.00**
- (ii) Uzio na *Landscape* **Tsh 700,000,000.00**
- (iii) Samani za Ofisi **Tsh 500,000,000.00**